OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

SHULE YA SEKONDARI MOIPO,
S. L. P 61,
SAME.
TAREHE 17/12/2020

KUMB. NA. MSS/A1/8/17

JINA LA MWANAFUNZI……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Moipo mwaka 2021. Kwa niaba ya Waalimu,Wafanya kazi,Wanafunzi na Jumuiya nzima ya shule hii, ninakupa pongezi na kukukaribisha kwa moyo wa dhati hapa shuleni.

Napenda pia kukukumbusha maneno ya mheshimiwa Baba wa taifa letu, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere na yale yasemwayo na viongozi wa Chama na Serikali kuhusu Elimu ya Sekondari kuwa kuchaguliwa kwako ni BAHATI na wala sio STAHILI au HAKI yako, na kuwa unalo deni kubwa kwa nchi yako. Ukija hapa ni kama uliyetumwa na wananchi, uje uvune chochote na kurudi kuwasaidia ulichovuna. Hili ndilo lengo lako kubwa kwa muda wote utakaokuwa hapa shuleni. Wajibu wako mkubwa ni kusoma kwa bidii, kufuata sheria na taratibu za shule, kushiriki katika elimu ya kujitegemea na kutekeleza yale yote mema utakayoelekezwa na wazazi, walimu na walezi wako.

2. SHULE ITAFUNGULIWA TAREHE 11/01/2021

3. MAHALI SHULE ILIPO:

Shule ipo Wilaya ya Same, Kata ya Ruvu, Kilometa 28 kutoka Same mjini kuelekea Ruvu Muungano. Iwapo unakubali uchaguzi huu, basi zingatia mahitaji na masharti muhimu yaliyotajwa hapa chini.

4. MAHITAJI MUHIMU:

A. MAVAZI:

1. **Wavulana**:Suruali mbili za rangi ya kijani kirichi na mashati mawili meupe(cotton-tomato) ya mikono Mifupi. (mzazi/mlezi ashone mwenyewe)
2. **Wasichana**:Sketi mbili za rangi ya kijani kirichi na mashati mawili meupe(cotton-tomato) ya mikono Mifupi. (mzazi/mlezi ashone mwenyewe)
3. **Kwa wote**:
   a) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu na kisigino kifupi.
   b) Soksi jozi mbili nyeupe ndefu(kwa wasichana) na soksi nyeusi kwa wavulana.
   c) Masweta Kijani kirichi.

NB: Suruali zishonwe ziwe na marinda (sio modal) na sketi ziwe na marinda madogo madogo sio marinda mapana.

B. VIFAA VYA MADARASANI:
a) Madaftari makubwa 10 (Counter Book 3or 4 quires) kwa ajili ya masomo.
b) Kopo la vifaa vya hisabati (Mathematical instruments' set).
c) Dictionary

C. **VIFAA VYA KAZI:**
a) **Kwa wanafunzi wote:** wanatakiwa kuleta ufagio wa njiti za mnazi (chelewa)

5. FOMU MUHIMU:

Pamoja na barua hii naambatanisha fomu A: Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi na B: Fomu ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi itakayojazwa na daktari wa Wilaya kuhusu afya ya mwanafunzi. Fomu hizi zijazwe kikamilifu na mwanafunzi aje nazo shule itakapofunguliwa na ikabidhiwe kwa mkuu wa shule.

6. 6.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE:

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu walimu na wafanyakazi wote na pia wanafunzi wenzake na wanajumuiya wote.

ii. Kushirikiana na kusaidiana katika kazi.
iii. Kuheshimu ratiba nzima ya shule.
iv. Mwanafunzi haruhusiwi kutenda yafuatayo:-
a) Kuvuta sigara, Bangi,kula mirungi au Madawa ya kulevya
b) Kufuga kucha, Nywele na ndevu.
c) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima kwa mfano sketi fupi kwa wasichana, suruali za kubana na mlegezo kwa wavulana.
d) Kugombana au kupigana
e) Kunyoa nywele mitindo ya kihuni.
f) Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya mwalimu
g) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.

6.2 MAHUDHURIO:

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ya darasani na ya nje ya darasa bila kukosa. Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria shuleni kwa siku 195 kwa mwaka.
ii. Kila mwanafunzi ni lazima kufanya mazoezi ya juma, majaribio ya mwezi na mitihani ya muhula kama itakavyoelekezwa.
iii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria miito na mikutano yote, kama Roll call, Inspections, Assembly n.k.
iv. Kutunza muda na ratiba ya shule (Ratiba nzima ya shule)
v. Mwanafunzi asipohudhuria masomo mzazi atawajibika. Hivyo ni jukumu la mzazi kushirikiana na walimu kuhimiza mtoto kuhudhuria shule.

6.3 <u>MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE</u>.

i. Wizi.
ii. Uasherati.
iii. Ulevi wa aina yoyote ile.
iv. Uvutaji bangi.
v. Makosa ya jinai.
vi. Kupigana au kupiga.
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
viii. Kudharau bendera ya Taifa.
ix. Kuoa au kuolewa.
x. Kumpa mimba msichana.
xi. Kupata mimba.
xii. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo.
xiii. Kutohudhuria vipindi vya masomo mfululizo bila sababu muhimu.
xiv. Kukataa adhabu.
xv. Kunyanyasa wanafunzi wengine.
xvi. Kulala nje ya shule kwa wanafunzi wa bweni/Hosteli bila ruhusa maalumu.
xvii. Kutembelea majumba ya starehe kwa mfano nyumba za kulala wageni, vilabu vya pombe, kumbi za muziki n.k
xviii. Kukamatwa na simu

Karibu sana Moipo Sekondari!
Nakutakia Mafunzo mema

_____
NURU M. MOHAMED
MKUU WA SHULE

FOMU A

SHULE YA SEKONDARI MOIPO
FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

A: <u>TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI</u>:

JINA LA MWANAFUNZI (LA MTIHANI) ……

TAREHE YA KUZALIWA …… MAHALI PA KUZALIWA ……

URAIA: MTANZANIA / SI MTANZANIA ……

SHULE ALIYOTOKA …….. NAMBA YA MTIHANI ……

JINA LA MZAZI/MLEZI ……

ANUANI YA MZAZI/MLEZI ……

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI ……

KAZI YA MZAZI/MLEZI ……

B: <u>KUKUBALI NAFASI NA MAELEZO ULIYOPEWA:</u>

Mimi ……. Wa kidato cha ……. Mwaka ……
Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo na kwamba nimekubali kupokea nafasi niliyopewa.

TAREHE …… SAHIHI ……

C: <u>KUKUBALI NA KUFUATA SHERIA ZA SHULE</u>:

Mimi …….. mwanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ……
Nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na ninaahidi kwamba nitazitii sheria zote, maelekezo na maagizo nitakayopewa na mwalimu na viongozi wa shule. Iwapo nitakwenda kinyume, nitawajibika kufuatana na sheria za shule.

TAREHE …… SAHIHI …….

<u>MZAZI</u>:

Mimi …… mzazi / mlezi wa mwanafunzi
……. Wa kidato cha kwanza mwaka …….
Nimesoma / Nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayohusu mwanafunzi ……
…… nakubali kushirikiana na walimu katika kumlea na kumshauri ipasavyo, na kutimiza mahitaji yake ya shule kwa manufaa yake binafsi na Taifa kwa ujumla.

TAREHE ……. SAHIHI ……

D: <u>MTENDAJI KATA</u>:

Mimi …… Mtendaji Kata ya ……
Nathibitisha kwamba mwanafunzi aliyetajwa hapo juu ni wa Kata yangu na kwamba ni mwanafunzi halali aliyechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Moipo.

TAREHE …… SAHIHI …….

FOMU B

UCHUNGUZI WA AFYA YA MWANAFUNZI

(Sehemu hii ijazwe na Daktari wa Hospitali ya Serikali)

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI MOIPO
S. L. P 61, SIMU: 0786 762447, SAME

TO MEDICAL OFFICER,
…….
…….

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR ……..

Please examine the above named student as his / her physical and mental fitness for pursuing the Secondary School Education. The medical Examination should include the following areas:

1. **Eye Sight ……...**
2. **Hearing …….**
3. **Leprosy …….**
4. **Limbs ……**
5. **Epilepsy ……**
6. **Asthma ……**
7. **T.B …….**
8. **Neurosis ……**
9. **Other diseases (if any) …….....**
   ……
   ……

MEDICAL CERTIFICATE

I certify I have examined the above named student and consider him/her physical and mentally fit / unfit to pursue studies at Secondary Level.

Station …….

Designation …….

Signature …….
and

Medical Officer Stamp

Date ……